



Siku niliyo ondoka nyumbani
kuelekea jijini!



✎ Lesley Koyi, Ursula Nafula
👤 Brian Wambi
📧 Ursula Nafula
😊 Kiswahili
📖 Level 3




Storybooks Canada

storybookscanada.ca

Siku niliyo ondoka nyumbani kuelekea
jijini!

Written by: Lesley Koyi, Ursula Nafula
Illustrated by: Brian Wambi
Translated by: Ursula Nafula

This story originates from the African Storybook
(africanstorybook.org) and is brought to you by
Storybooks Canada in an effort to provide
children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0).
<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0>



Kituo kidogo cha mabasi kijijini mwetu kilijaa shughuli za watu na mabasi. Basi nyingi zilikuwa zimejaza mizigo. Chini, palikuwa na mizigo zaidi ya kupakia. Kondakta waliita majina tofauti ya mahali basi zilielekea.



“kwenda jijini! kwenda jijini! kwenda magharibi!” Nilisikia kondakta akita kwa sauti. Ile ndiyo basi niliyohitaji kupanda kwa usafiri wangu.



Basi la kwenda jijini lilikuwa karibu kujaa, lakini watu zaidi walijishughulisha kutaka kupanda. Baadhi yao walipakia mizigo chini ya basi. Wengine waliweka katika sehemu ya juu.





Basi la kurudi lilikuwa linajaa upesi. Muda mfupi baadaye, lingeanza safari ya kwenda mashariki. Jambo la maana kwangu wakati huo lilikuwa kuanza kutafuta nyumba ya mjomba wangu.

Abiria wapya walishika tiketi zao huku wakitafuta mahali pa kukaa. Wanawake waliokuwa na watoto wodogo waliwatayarisha kwa safari hiyo ndefu.



Bada ya saa tisa, niliamshwa kwa kelele za kita abiria waliokwenda katika kijiji changu. Nilichukuwa mfuko wangu mdogo na kuruka nje ya basi.





Nilipenyeza ndani nikakaa karibu na dirisha. Mtu aliyeketi karibu nami alishika mfuko wa plastiki wa kijani kibichi. Alivaa viatu vilivyozeeka, koti kukuu na alionekana kuwa na wasiwasi.



Njiani, nilikariri jina la mahali mjomba wangu alipoishi katika jiji kubwa. Nilikuwa bado nafikiria wakati nilipopatwa na usingizi.



Niliangalia nje na kutambua kwamba
niliikuwa naondoka kijijini mwangu, mahali
ambapo nililelewa. Niliikuwa naenda katika
jiji kubwa.



Lakini mawazo yangu yalirejea nyumbani.
Je, mamangu atakuwa salama? Je, sungura
wangu wataleta hela zozote? Je, ndugu
yangu atakumbuka kunyunyizia maji
miche ya miti yangu?



Upakiaji mizigo ulikamilika na abiria wakawa wameketi. Wachuuzi walizidi kusukumana kutaka kuingia ndani ya basi ili wauze bidhaa zao. Kila mmoja alitaja kwa sauti majina ya bidhaa alivyokuwa anauza. Maneno yao yalinifurahisha.



Safari ilipoendelea, joto lilikuwa jingi ndani ya basi. Niliyafumba macho yangu nikiuia kulala.



Baadh! ya abiria walinnua vinywaji.
Wengine wakanua vitafunwa vidogo na
kuanza kutafuna. Wasiokuwa na fedha,
kama mimi, walitazama tu.



Basi lilipoondoka kituoni, nilichungulia
dirishani. Nilijuliza endapo ningrudi na
kwenda kijijini kwangu tena.



Shughuli hizi zilikatizwa kwa mlio wa honi ya basi, ishara kwamba tulikuwa tayari kuondoka. Kondakta aliwataka wachuuzi kuondoka ndani ya basi.



Wachuuzi walisukumana huku wakitafuta njia ya kushuka. Wengine wao waliwarudisha abiria chenji zao. Wengine walifanya juhudi za mwisho kuuza bidhaa zao.